

# ARU BULLETIN

PREPARED BY COMMUNICATION AND MARKETING UNIT

VOLUME: 02

## JARIDA MAALUM

**KONGAMANO LA SIKU YA WANAWAKE DUNIANI**

INDEX
KONGAMANO LA WANAWAKE CHUO KIKUU ARDHI LAFANA | PROF.LIWA KONGAMANO | ELIMU YA USIMAMIZI WA FEDHA

# KONGAMANO LA WANAWAKE CHUO KIKUU ARDHI LAFANA

Kuelekea Siku ya Wanawake Duniani, watumishi wanawake wa Chuo Kikuu Ardhi tarehe 3.03.2023 wamefanya Kongamano lenye lengo la kukumbushana mambo mbalimbali yanayohusu ustawi wa kazi Chuoni.

Kongamano hilo lilianza kwa Maandamano yaliyoanzia jengo la Utawala kuelekea Viwanja vya ARISA ambapo waandamanaji waliimba nyimbo mbalimbali zenye kuhamasisha Ari ya wanawake kwenye ufanyaji kazi na kuchukua majukumu muhimu kwenye ngazi ya familia, kazini na Taifa kwa ujumla

Aidha Kongamano hilo lilifuatiwa na Semina ambapo Mgeni rasmi katika semina hiyo alikuwa ni Makamu Mkuu wa Chuo Prof. Evaristo Liwa ambae aliwapongeza wanawake kwa kufanya kazi kwa umahiri iliyopolekea kuwa na idadi kubwa ya viongozi wanawake katika ngazi ya Menejimenti.



> "Mmekuwa mkifanya kazi inayoonekana, sina shaka na utendaji wenu ambao umepelekea wengi wenu kuwa viongozi wa ngazi za juu hapa Chuoni." Alisema Prof. Liwa wakati wa ufunguzi wa Semina hiyo.

Nae Bi. Lydia Gunzu ambae ni Mratibu Mkuu kamati ya Wanawake tawi la ARU - THTU amesema, semina hiyo imeandaliwa ili kukumbushana mambo muhimu ambayo yatasaidia katika kuboresha utendaji kazi Chuoni.

Amesema mada zote zilizowasilishwa zimeendana na Kauli mbiu ya mwaka huu ambayo ni **"Ubunifu wa mabadiliko ya teknolojia, chachu katika kuleta usawa wa kijinsia"**

Katika semina hiyo mtoa mada Bi. Julieth Mchunguzi kutoka Taasisi ya Ustawi wa Jamii aliongelea kuhusu afya ya akili huku Bwn. Husama Nurdin wa Idara ya mafunzo ya Biashara kutoka Chuo Kikuu Ardhi aliongelea maswala ya usimamizi wa fedha na maandalizi kabla ya kustaafu



# PROF. LIWA AWAASA WATUMISHI WANAWAKE KUSHIRIKI MALEZI YA WANAFUNZI WA CHUO KIKUU ARDHI

Makamu Mkuu wa Chuo Prof. Evaristo Liwa amewaasa watumishi wanawake wa Chuo Kikuu Ardhi kushiriki kikamilifu katika malezi ya wanafunzi wa Chuo Kikuu Ardhi ili kusaidia kukabiliana na mabadiliko ya kitabia yanayotokana na mtindo wa maisha wa sasa unaosababishwa na utandawazi. Utandawazi pamoja na sababu nyingine umepelekea kuwaweka vijana katika hatari ya kutumbukia katika dimbwi la mmomonyoko wa maadili kwa kuiga tamaduni za kigeni ambazo ni fedheha kwa taifa la Tanzania na Afrika kwa ujumla.



Prof. Liwa ameyasema hayo wakati wa ufunguzi wa Semina maalumu ya Wanawake wa Chuo Kikuu Ardhi iliyofanyika tarehe 03.03.2023, ikiwa ni shamra shamra za kuelekea Siku ya Wanawake Duniani.

Prof. Liwa amesema kuwa Wanawake wana mchango mkubwa katika kuboresha malezi ya vijana wa kike na wa kiume na hivyo kufanikisha mustakabali i mzuri wa tabia za wanafunzi ukizingatia kuwa vijana wengi hapa Chuoni wanatarajiwa kuwa viongozi wa baadae katika nyanja mbalimbali ikiwemo Siasa, Elimu, Uchumi na ngazi ya Jamii.



> Viongozi jengeni utaratibu wa kuzungumza na vijana mara kwa mara ili waelewe umuhimu wa nafasi zao katika jamii na kuendelea kusimama katika misingi iliyo bora. Tutakaporudi mwakani kwenye semina kama hii nitaomba kupewa taarifa ya hatua zilizochukuliwa na vikao vilivyokaa kuwajumuisha wanafunzi kuhusiana na suala la mmomonyoko wa maadili. Hii ni katika kuhakikishakwambaChuo chetu hakiwi mfano wa mahali pa kulea vijana wenye tabia potofu.
> alisema Prof. Liwa.



Mbali na hayo, Prof. Liwa aliwapongeza wanawake wote wa Chuo Kikuu Ardhi kwa kuandaa semina hiyo ambayo mbali na kukumbushana masuala mbalimbali pia inawajengea ukaribu baina yao na kuweza kutatua changamoto zinazowakabili ili kuleta ari ya ufanyaji kazi wenye tija Chuoni





## MATUKIO NA PICHA








# ELIMU YA USIMAMIZI WA FEDHA YATOLEWA KWA WANAWAKE CHUO KIKUU ARDHI

Watumishi Wanawake Chuo Kikuu Ardhi wamepatiwa Elimu juu ya Usimamizi wa fedha ambayo itawasaidia katika upangaji mzuri wa shughuli za kujipatia na kujiongezea kipato lakini pia namna bora ya kufanya matumizi ya fedha wanazozipata kwa vyanzo mbalimbali ikiwemo fedha zinazotokana na mishahara.

Akizungumza wakati wa uwasilishaji wa mada hiyo Mkufunzi CPA Husama Nurdini Igangula Mtaalamu kutoka Idara ya Mafunzo ya Biashara ya Chuo Kikuu Ardhi amesema, ili kuwa na mtindo mzuri wa usimamizi wa fedha (bajeti binafsi) ni vyema kufuata kanuni ya 50%, 30% na 20% ambapo mgawanyo huo ni kutokana na kipato cha kila Mtumishi kwa mwezi ambapo 50% itahusisha matumizi ya muhimu na lazima (basic needs) kama vile Malazi, Chakula, maji na Mavazi, pia mahitaji mengine muhimu kama nauli au gharama ya usafiri, mawasiliano, bima nakadhalika, 30% ni (wants), kimsingi haya ni matumizi ya ziada ili kuongeza furaha ya moyo na kuburudika kama vile kula chakula cha bei ya juu kwenye migahawa, kutoka na kula chakula cha usiku (dinner), kufanya urembo wa kucha, saluni, kwenda sinema, kununua mkoba mpya, kununua simu za kisasa kila toleo jipya linapo kuja sokoni, kununua vitu vyenye majina (branded products), kutekeleza hobi zako na aina nyingine za kuupa mwili pole na kumwagilia roho, huku 20% ikiwa ni malengo ya kifedha ikiwemo kuwekeza, kuweka akiba (savings), kuwa na mfuko wa dharura (emergence fund), kuweka mfuko wa fedha kwaajili ya kusherekea sikukuu au siku ya kuzaliwa, kuweka akiba kwa ajili ya kustaafu.

Amesema changamoto inatokea pale mtu anavyofanya matumizi makubwa katika mahitaji ambayo si ya lazima huku matumizi ya msingi yakiachwa. Akijibu swali kutoka kwa mjumbe aliyetaka kujua kuhusu kiasi cha pesa kinachofaa kwa Mtumishi kukopa Benki ili aweze kupata mtaji wa biashara, CPA Nurdini alisema, si vyema kutumia kiasi chote (100%) cha mkopo wa Benki kwa ajili ya kuanzisha biashara kwani dira ya biashara inaweza kupotea kwa sababu italazimu kutilia mkazo kufanya marejesho badala ya kuendeleza biashara, hivyo fedha ya kuanza biashara/mtaji (seed capital) kwa uchache asilimia hamsini (50%) ni vyema ukatokana na akiba zako au fedha kutoka kwa ndugu au familia.



CPA Husama Nurdini Igangula
Mtaalamu kutoka Idara ya Mafunzo ya Biashara ya Chuo Kikuu Ardhi

# ELIMU YA USIMAMIZI WA FEDHA YATOLEWA KWA WANAWAKE CHUO KIKUU ARDHI

> "Biashara inahitaji akili iliyotulia ili kuweza kujiendeleza zaidi, kwani inahitaji ubunifu wa mara kwa mara unaoendana na kuongezeka kwa mtaji, ukiwa na mkopo mkubwa itakulazimu pia kutumia kiasi kikubwa kwa ajili ya kulipia mkopo hivyo kupelekea biashara kudumaa au kufa kabisa endapo kutatokea changamoto mbalimbali kama vile magonjwa ya mlipuko na majanga mengine ya asili" Alisema CPA Nurdin.





Wakati huo huo pia amewaasa Watumishi kuanza mapema kujishughulisha na shughuli ndogo ndogo za kujiongezea kipato kwa wakati wao wa ziada, shughuli ambazo hata wakati wa kustaafu, watakuwa na uzoefu nazo na hivyo watazifanya kwa ufanisi mkubwa kuliko kusubiri kuanza shughuli hizo mara baada ya kustaafu.



# WANAWAKE CHUO KIKUU WAPONGEZWA KWA KUSIMAMIA VYEMA MAJUKUMU YAO

Wanawake Chuo Kikuu Ardhi wamepongezwa kwa kuendelea kusimamia vyema majukumu yao ya kazi na uongozi Chuoni ambapo imeelezwa kuwa 60% ya nafasi za uongozi zinashikiliwa na Wanawake ambao wamethibitika kufanya vyema katika utekelezaji wa majukumu yao.

Ameeleza Bi Lydia Guzu ambae ni Mratibu Mkuu kamati ya Wanawake tawi la THTU Chuoni hapo wakati akisoma houtuba yake ya ukaribisho kwenye Semina maalumu ya Wanawake kuwa, Kazi nzuri zinazofanywa na viongozi wanawake inadhihirisha wazi kuwa Wanawake wanauwezo mkubwa wa kuleta maendeleo kwani wana uthubutu na pia wana dhamira thabiti ya kuona Chuo kinazidi kusonga mbele.



> "Wanawake ni jeshi kubwa na imara, najivunia sana kuona wanawke wenzangu mlio wengi mmeshika nyadhifa kubwa hapa Chuoni na kwa kiasi kikubwa mmezitendea haki nyadhifa hizo kwa viwango vya hali ya juu" alisema Bi Lydia Gunzu.

Nae Mgeni Rasmi Katika Semina hiyo Prof. Evaristo liwa amesema, wanawake wanaoshika nyadhfa mbalimbali Chuoni, wamejipambanua kwa uwezo wao mzuri wa kazi na si kwa upendeleo. Ametaja baadhi ya maeneo ambayo wanawake ni viongozi ni pamoja na Shule zote Nne za Chuo, Idara ya Elimu endelevu ( Center for Continuing Education), Kurugenzi ya Utawala na Usimamizi wa Rasilimali watu, Kitengo cha Sheria, Kitengo cha Ukaguzi wa ndani, Kitengo cha Manunuzi na Kitengo cha Mwasiliano na Masoko.

Prof. Liwa ametoa rai kwa viongozi hao na wafanyakazi wote kwa ujumla kuendelea kufanya kazi kwa weledi na ushirikiano ili kukiletea Chuo mafanikio makubwa zaidi.



Bi Lydia Guzu - Mratibu Mkuu kamati ya Wanawake tawi la THTU





## MATUKIO NA PICHA













